# Picha za Matukio mbalimbali ya Mkutano Mkuu wa Tano wa mwaka wa TGDC



Picha za Matukio mbalimbali ya Mkutano Mkuu wa Tano wa mwaka wa TGDC (5th Annual General Meeting) uliofanyika tarehe 17.08.2023 katika ukumbi wa mikutano wa kimataifa wa Mwalimu Nyerere. Mkutano huo uliongozwa na Prof. Shubi Felix Kaijage (Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TGDC). Katika Mkutano huo Mwanahisa (Shareholder) ambaye ni Kampuni ya TANESCO iliwakilishwa na Bodi yake ya Wakurugenzi chini ya uongozi wa Ndugu Omari Issa



# Picha za Matukio mbalimbali ya Mkutano Mkuu wa Tano wa mwaka wa TGDC







# Picha za Matukio mbalimbali ya Mkutano Mkuu wa Tano wa mwaka wa TGDC









# Picha za Matukio mbalimbali ya Mkutano Mkuu wa Tano wa mwaka wa TGDC







# USHIRIKI WA TGDC KATIKA NANENANE MBEYA:

Toleo la Nanenane

Agosti 2023



Katika kuendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi imeendelea mwezi huu. Hayo yalijiri wakati Shirika la Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) ilivyoshiriki kwa mafanikio makubwa katika maonesho ya Nanenane, ambayo yalifanyika kitaifa mkoani Mbeya. Maonesho haya yamekuwa jukwaa muhimu la kukuza hatua za kimaendeleo na kuonyesha mafanikio ya sekta mbalimbali nchini na ikitupa TGDC nafasi ya kujitangaza.

Katika maonesho hayo, TGDC ilijitokeza kwa nguvu na kujenga uwezo na uelewa kwa wananchi wa mkoani Mbeya juu ya sekta ya nishati ya jotoardhi. Kupitia mabanda yao maalum, TGDC ilitoa elimu kwa wageni kuhusu faida za jotoardhi na jinsi teknolojia hii ya kisasa inavyoweza kuchangia katika ustawi wa nchi yetu kama nishati mbadala. Mbali na kutoa elimu, TGDC pia iliwapa washiriki wa maonesho fursa ya kuona na kujifunza vifaa vya teknolojia ya jotoardhi.

Pia, walitoa maelezo ya kina kuhusu miradi ya kimkakati na hatua mbalimbali zilizofikiwa katika uendeleshaji wa nistati ya jotoardhi nchini, ikiwa ni pamoja na jinsi wanavyoshirikiana na wadau wengine kukuza na kuendeleza matumizi ya nishati hii safi na salama.

Ushiriki wa TGDC katika maonesho ya Nanenane unaonyesha dhamira yao ya kuchangia katika maendeleo ya nishati hasa kwa upande wa nishati jadidifu yaani jotoardhi nchini Tanzania. Kutambulisha teknolojia hii kwa umma na wadau husika ni hatua muhimu katika kufikia malengo ya nishati safi na endelevu. Kushiriki katika maonesho haya ni ishara ya dhamira yao ya kukuza uelewa na kuwajengea watu uwezo katika matumizi ya moja kwa moja na yale yasiyo moja kwa moja na faida za jotoardhi.

TGDC inaendelea kujitahidi kuwa mhimili wa maendeleo ya nishati ya jotoardhi nchini, hilo limethibitishwa kwa uongozi wao katika sekta hii muhimu na kuonyesha umuhimu wa nishati hii safi na endelevu kwa mustakabali wa Tanzania.



# USHIRIKI WA TGDC KATIKA NANENANE MBEYA:




**MBUNGE WA MALINYI, ANTIPAS MNGUSI AKIWA ANAPATIWA MAELEZO MBALIMBALI KUTOKA KWA *MANAGER GEOSCIENCE* ALBANO MAHECHA ALIVYOTEMBELEA BANDA LA TGDC LEO KATIKA MAONESHO YA NANENANE MKOANI MBEYA**




**FUNDI MCHUNDO HERIEL THOMAS AKIWA NA WANAFUNZI WA VYUO MBALIMBALI AMBAO WAPO TGDC WAKIPATA ELIMU KWA VITENDO WALIPOTEMBELEA BANDA LA TGDC.**

# USHIRIKI WA TGDC KATIKA NANENANE MBEYA:




**TIMU YA TGDC IKIWA INAWAHUDUMIA NA KUWAPA ELIMU KUHUSIANA NA JOTOARDHI WADAU MBALIMBALI WALIOJITOKEZA KATIKA MAONESHO YA NANENAN.**



**KATIKA PICHA NI WATOTO MBALIMBALI AMBAO WAMEPATA KUTEMBELEA BANDA LETU LA TGDC ILI KUJIFUNZA MAMBO MBALIMBALI KUHUSIANA NA JOTOARDHI.**

# USHIRIKI WA TGDC KATIKA NANENANE MBEYA:



WADAU MBALIMBALI KATIKA PICHA WALIVYOTEMBELEA BANDA LA TGDC KATIKA MAONESHO YA NANENANE KUPATA ELIMU NA MAARIFA KUHUSIANA NA JOTOARDHI NA MIRADI YA KIMKAKATI INAYOENDELEA KUTEKELEZWA NCHINI.




KATIKA PICHA NI WATOTO MBALIMBALI AMBAO WAMEPATA KUTEMBELEA BANDA LETU LA TGDC ILI KUJIFUNZA MAMBO MBALIMBALI KUHUSIANA NA JOTOARDHI.

# TANZANIA INAENDELEA KUTAFUTA WAWEKEZAJI WA NISHATI YA JOTOARDHI KWA KAMPUNI YA TOSHIBA , JAPAN.



Mha. Innocent Luoga, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu wa Wizara ya Nishati akiongoza kikao cha ujumbe wa Tanzania na wawakilishi wa Kampuni ya TOSHIBA kwa ajili kujadili namna bora ya Kushirikiana katika kuendeleza Nishati ya Jotoardhi nchini Tanzania. Katika ziara hiyo Kamishna Luoga ameambatana na Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Bw. Petro Lyatuu, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TGDC, Prof. Shubi Kaijage na Kaimu Meneja Mkuu wa TGDC, Mha.Mathew Mwangomba. Katika kikao hiki Wawekezaji kutoka TOSHIBA Bw. Kosuke Shibata(Deputy Commercial Manager), Bw. Hideyuki Morii (Deputy Commercial Manager) na Bw. Toyoaki Fujita (Business Development Executive)



Programu hii ambayo ilikuwa ya siku nane imeandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO) kwa lengo la kuimarisha utaalamu wa washiriki katika uendelezaji wa rasilimali za jotoardhi pamoja na ugharamiaji wa miradi ya kuzalisha umeme kupitia jotoardhi. Aidha, kupitia programu hii, washiriki wameweza kukutana na Taasisi za Ushauri, Wawezekaji na Taasisi mbalimbali za Fedha kwa ajili ya kujadili namna bora ya kuendeleza miradi ya jotoardhi.

# TANZANIA INAENDELEA KUTAFUTA WAWEKEZAJI WA NISHATI YA JOTOARDHI KWA KAMPUNI YA TOSHIBA , JAPAN.



Tanzania inakadiriwa kuwa na MW 5,000 za nishati ya za kuzalisha umeme katika maeneo Zaidi ya 50 yaliyoainishwa na Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania TGDC zitakapokamilika kufanyiwa kazi. Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi ina jukumu la kuzalisha umeme kwa kutumia rasilimali hiyo, ambapo matarajio ni kuzalisha MW 200 itakapokamilika miradi yote ya kimkakati ya jotoardhi Ngozi MW 70, Kiejo – Mbaka MW 60, Natron MW 60, Songwe MW 5 na Luhoi MW 5.



# KAMISHNA WA UMEME NA NISHATI JADIDIFU AONGOZA UJUMBE KUTOKA TANZANIA NCHINI JAPAN NA WAWAKILISHI WA KAMPUNI YA TOSHIBA KUJADILI UENDELEZAJI WA NISHATI YA JOTOARDHI.



Mha. Innocent Luoga, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu wa Wizara ya Nishati akiongoza kikao cha ujumbe wa Tanzania na wawakilishi wa Kampuni ya TOSHIBA kwa ajili kujadili namna bora ya Kushirikiana katika kuendeleza Nishati ya Jotoardhi nchini Tanzania. Katika ziara hiyo Kamishna Luoga ameambatana na Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Bw. Petro Lyatuu, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TGDC, Prof. Shubi Kaijage na Kaimu Meneja Mkuu wa TGDC, Mha.Mathew Mwangomba. Katika kikao hiki Wawekezaji kutoka TOSHIBA Bw. Kosuke Shibata(Deputy Commercial Manager), Bw. Hideyuki Morii (Deputy Commercial Manager) na Bw. Toyoaki Fujita (Business Development Executive)



Programu hii ambayo ilikuwa ya siku nane imeandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO) kwa lengo la kuimarisha utaalamu wa washiriki katika uendelezaji wa rasilimali za jotoardhi pamoja na ugharamiaji wa miradi ya kuzalisha umeme kupitia jotoardhi. Aidha, kupitia programu hii, washiriki wameweza kukutana na Taasisi za Ushauri, Wawezekaji na Taasisi mbalimbali za Fedha kwa ajili ya kujadili namna bora ya kuendeleza miradi ya jotoardhi.

# KAMISHNA WA UMEME NA NISHATI JADIDIFU AONGOZA UJUMBE KUTOKA TANZANIA NCHINI JAPAN NA WAWAKILISHI WA KAMPUNI YA TOSHIBA KUJADILI UENDELEZAJI WA NISHATI YA JOTOARDHI.



Tanzania inakadiriwa kuwa na MW 5,000 za nishati ya za kuzalisha umeme katika maeneo Zaidi ya 50 yaliyoainishwa na Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania TGDC zitakapokamilika kufanyiwa kazi. Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi ina jukumu la kuzalisha umeme kwa kutumia rasilimali hiyo, ambapo matarajio ni kuzalisha MW 200 itakapokamilika miradi yote ya kimkakati ya jotoardhi Ngozi MW 70, Kiejo – Mbaka MW 60, Natron MW 60, Songwe MW 5 na Luhoi MW 5.



# UJUMBE WA TANZANIA KUTOKA WIZARA YA NISHATI NA TGDC WATEMBELEA UBALOZI WA TANZANIA NCHINI JAPAN



Mha. Luoga na ujumbe wake wanaudhuria programu ya siku nane ambayo imeandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO) kwa lengo la kuimarisha utaalamu wa washiriki katika uendelezaji wa rasilimali za jotoardhi pamoja na ugharamiaji wa miradi ya kuzalisha umeme kupitia jotoardhi. Aidha, kupitia programu hii, washiriki wameweza kukutana na Taasisi za Ushauri, Wawezekaji na Taasisi mbalimbali za Fedha kwa ajili ya kujadili namna bora ya kuendeleza miradi ya jotoardhi. Tanzania ina rasilimali za jotoardhi zinazoweza kuzalisha umeme wa zaidi ya MW 5,000 katika maeneo yaliyoainishwa.

